

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NNE**

**04 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA NNE – TAREHE 04 JUNI, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### III. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

#### 367. MHESHIMIWA VEDASTUS MATHAYO MANYINYI (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kupunguza tatizo la ukosefu wa Ajira kwa Vijana wanapomaliza Vyuo Vikuu;

(b) Je, ni kwa nini Vijana hao wasitumie Vyeti vyao kama dhamana kupata mikopo ili wajishughulishie na shughuli mbalimbali za Kiuchumi.

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 368. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mtwara.

**369. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Maboma ya Shule za Sekondari Bombo na Ndungu ili Kidato cha Tano kianze baada ya Mabweni ya Wasichana kukamilika.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**370. MHESHIMIWA ASSA NELSON MAKANIKA (KIGOMA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itawasaidia Wananchi wa Kigoma ambao wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara kwa kuitwa Wakimbizi nchini mwao.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**371. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-



Je, ni lini Serikali itanza ujenzi wa Barabara ya Handeni, Mziha hadi Turiani Morogoro.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**372. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itafanya Marekebisho ya Malengo ya Mtaala wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini ili kuendana na uhitaji wa sasa.

**WIZARA YA MAJI:**

**373. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itanza Mradi wa kuyatoa Maji toka Ziwa Tanganyika na kuyapeleka katika Manispaa ya Mpanda.

**374. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika Mradi wa kutoa Maji kutoka Nzega Mjini tenki la Ushirika hadi Bukene ambapo Vijiji 20 na Vitongoji zaidi ya 100 vitanufaika.

**375. MHESHIMIWA ALEXANDER PASTORY MNYETI (MISUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itamaliza changamoto ya Maji katika Kituo cha Utafiti na Chuo cha Kilimo Ukirigulu.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**376. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Majengo ya Mahakama za Mwanzo katika Kata za Nkoanrua na Nkoaranga ambazo majengo yake yamebomoka.


**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA**  
**04 JUNI, 2021**



**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**